MWITO PROGRAM KISWAHILI SCRIPT

PROGRAM NUMBER 1133

SCRIPTURE:ROMANS 8 :12

DURATION:15 MINUTES.

Ni furaha kuu msikilizaji wangu kukukaribisha kwenye kipindi cha Mwito ambacho hukujia saa na wakati kama huu kupitia idhaa hii.Madhumuni ya kipindi hiki ni kukuelimisha na kukujumuisha katika kundi la wale walio na hamu ya kueneza injili ya wokovu ya Yesu Kristo.Kaa tayari manake mwishoni mwa kipindi hiki nitakupatia simu ya mawasiliano na jinsi unavyoweza kujipatia agano jipya la Bibilia takatifu.Kwa mara nyingine tena nakukumbusha kuwa kipindi hiki kinakujia kwa hisani na ufadhili wa huduma ya kimataifa ya Macedonian Call yake mchungaji Harold Williams.Tunashukuru huduma hiyo na wengine ambao wamejitolea kuhakikisha kuwa unapokea mfululizo wa vipindi hivi kwa gharama yao.Kumbuka rafiki yangu gharama ya kununua muda wa kurushia vipindi hivi ni kubwa,ndiposa twawapa shukrani wafadhili wetu.Nakukumbusha ndugu msikilizaji kwamba kipindi hiki ni nambari 1132.Uko huru kuagiza vijitabu vya kujisomea ili kuimarisha imani yako.Tutajaribu kukutumia cho hote tulicho nacho mradi tu utupiie simu ,utuandikie arafa au kutuandikia kwa anwani nitkyokuatia mwisho wa kipindi hiki.Tunaendelea na somo leu na jinsi nilivyosema awali tunaendelea kuichambua sura ya 8 ya kitabu cha Warumi.Kwenye

kipindi kilichopita tulisoma aya ya 10-11 na 10 na leo tutaitizama aya ya 12.Naomba tuisome aya ya 11 na kuiambatanisha na ile ya 12 ambayo ndiyo ya leo *Aya ya 10 inasema…****Na kristo akiwa ndani yenu,mwili wenu umekufa kwa sababu ya dhambi; bali roho yenu i hai ,kwa sababu ya haki.***

Aya ya 11…..Lakini ikiwa roho yake aliyemfufua Yesu katika wafu aakaa ndani yenu,yeye aliyemfufua Kristo Yesu katika wafu atahuisha na miili yenu iliyo katika hali ya kufa,kwa Roho wake anayekaa ndani yenu.

Ndugu msikilizaji hebu sasa baada ya kusoma vifungu vya kiindi kilichopita ili upate ufhamu zaidi,tusome sasa aya ya 12 ya Warumi sura ya 8… ***Basi kama ni hivyo ndugu tu wadeni ,si wa mwili tuishi kwa kufwata mambo ya mwili….vs.13…Kwa maana tukiisi kwa kufuata mambo ya mwili,mwataka kufa;bali kama mkkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho,mtaishi.***

Naam hilo ni tamko la hakika.Kwamba sisi tu wadeni,sio kwa mwili,ili tuishi kama watumwa wa mwili.Kuna baadhi ya watu wanaofikiri kuwa inawabidi kuwa na wakati mzuri kwa mwili.Kwamba nimefanya kazi ngumu ,labda nijistareheshe nitakavyo.Wengi hawajui kuwa huo ni mtego mkubwa.Hawajui kuwa huo ni mtego mkubwa aliouweka shetani ili katika hizo starehe ukaingie kwenye majaribu ya anasa za dunia.Ninafahamu kuna namna tunavyoweza kujistrehesha lakini stare ambayo itampendeza Mungu pia.Starehe ambayo haitaathiri hali yako ya

kiroho.Mtume Paulo anasema kwa hivyo ninyi si wadeni tena kwa mambo ha mwili,bali wadeni kwa Yesu Kristo.Mu wadeni kwa wengine pia.Kuwaambia wengine kuhusu njia ya wokovu ya Kristo.Kuna huduma za udenezaji ninjli kama hii ya Macedonian Call,ambayo jukumu lake ni la kimishenari.Hivi ndivyo mtume Paulo alivyoweka katika sura ya kwanza **ya Warumi na nadhani aya ya 15**…***Kwa hiyo kwa upande wangu mimi ni tayari kuihubiri injili hata na kwenu ninyi mnaokaaa Rumi.Kwa maana sionei haya injili;kwasababu ni uweza wa Mungu uletao wokovu,kwa kila aaminiye,kwa myahudi kwanza na kwa myunani pia.***

Mtume Paulo alijisikia kuwa ana deni kubwa la kueneza injili kwa watu wote.Waeupe,weusi,wa njano na wa kila rangi na kila taifa.Mtume Paulo alikuwa anahizika kwenda hadi Hispania na hata mashariki ya mbali kupeleka injili pamoja na Rumi ambako alitumia muda wake mwingi.Alisema alikuwa deni kwa makanisa ma binadamu wote kupeleka injili na uhakikisha watu wanapata injili hii.Aidha alisema alikuwa na deni kwa Kriso ambaye kwa damu yake alipata msukumo wa kupeleka habari njema za wokovu.Kwa lugha ya kigiriki ,ambayo ilitumika kuandika agano jipya la Biblia neno hilo ni ***Oflatase*** ambalo lina maana ya kujukumika na kuwajibikia shughuli ya kufanya kitu au kutenda jambo fulani.Ndiposa Paulo anasema sisi tu wadeni.Mtume Paulo anataka twajibikie hilo na kuja mbele zake kumtumikia kwa furaha.Ujumbe wa Mtume Paulo ni kwamba uenende kila mahali

kuihubiri injili ya wokovu kwa wote tangia Judea hadi Samaria na hata pembe zote za ulimwengu.Tuenende kukaishi pamoja nao na kuwabiria injili wale ambao hawajaisikia.Na kama ilivyo chumvi,sisi ndisi chachu ya upelekaji wa injili kwa wote duniani.Ndisi nuru ya ulimwengu tuangaze gizani ili watu waone nuru;watoke gizani hadi nuruni.Kutoka Yerusalemu hadi Judea na hata Samaria na mwisho wa dunia wote wakalisikie neno hili la uzima.Ni sharti tufanya kazi ya Bwana kani dedni letu si la kimwili bali ni kwake Mungu.Tunatiwa nguvu na Roho wa Bwana kutenda kazi yake Mungu.Aya ya 13 inasema kuwa***…..Kwa maana kama tukiishi kwa kufwata mambo ya mwili;mwataka kufa;bali kama mkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho ,mtaishi.***

Maandiko hayasemi kufisha mwili bali kuyafisha matendo ya mwili kwa Roho,mtaishi.Bila shaka kuna utofauti mkubwa unaojitokeza wakati ambapo wakristo wanafisha matendo ya mwili na badala yake kuyazingatia yalio ya Mungu.Yesu alisema kuwa alikuja ili tuwe sio tu na na uzima bali uzima teletele.Mungu anataka mimi na wewe tuishi maosha ya utele,kwa kufisha matendo ya mwili.Ni dhahiri kwamba kuishi kwa matendo ya mwili kunaweza kupunguza urefu wa maisha yako.Hata hivyo nina ushuhuda wa waaminio wazuri sana ambao Mungu aliamua kuchukua uhai wao mapema kuliko ilivyo kawaida.

Naomba ufungue ami aya ya 14……Kwa kuwa wote wanaongozwa na Roho wa Mungu,hao ndio wana wa Mungu.Kwa kuwa hamkupokea tena

roho wa utumwa iletayo hofu;bali mlipokea roho ya kufanywa wana ambayo kwa hiyo twalia Aba,yaani Baba.

Nam mpendwa singpenda kuendelea zaidi ya hapo kwa leo.Ila natamsatisha kipindi kwa kuukuliza ikiwa haya niliyoyasema yana mana gani kwako.Umevifiisha viungo vya msili wako visitende yasiompndeza Mungu? Yaani umempokea Kristo kuwa mwokozi wa Roho yako? Ikiwa bado,fursa unayo leo.

Nakupa himizo leo ufanye hivho kwa kuzingatia na kuova nami hili ombi fupi la toba… Bwana Yesu,naja kwako nilivyo.nimetambua nimekuwa nikiishi maisha ya dhambi .Lakini sasa ninatubu.nisamehe dhambi zangu na unifanye kiumbe kipya.ingia ndani ya maisha yangu na kwa roho wako unifinyange na kunifanya kiumbe kipya utakavyo.katika jina la yesu nimeomba na kuamini .Amina.Ninamini ikiwa uliomba ombi hilo kwa kumanisha umeokoka na nkusihi umwendee mchungaji wako na kumfahamisha kuhusu uamuzi huo naye atakuelekeza jinsi ya kufanya.Ikiwa huhudhurii kanisa au huamini lolote kuhusu wokovu,basi mwendee mchungaji wa kanisa linaloamini injili ya wokovu ili akuombee na kukuelekeza kuhusu hatua ya kuchukua.Isitoshe waweza kutafuta ushauri kutoka kwa mwongofu yoyote yule ambaye atakusaidia kiroho.Na kufikia hapa sina budi kutamatisha kipindi hiki kwa leo.Jiunge nami kwa makala mengine ya kipindi kijacho cha MWITO.Hata hivyo nitakupatia maelezo na anwani yetu ili tuweze kudumisha uhusiano

wetu.Nitafurahi sana kuwasiliana nawe na ahata kukupatia vijitabu nan akala ya agano jipya la Bibilia kukusaidia kuweka msingi imara wa ukristo wako. Zaidi ya hayo.Nitafurahi sana nitakapopokea maoni yako kukihusu kipindi hiki na hasa jinsi ya kukifanya kiwe cha manufaa zaidi kwako.Hiki kimekuwa kipindi cha Mwito nambari 1133.Naomba uwasiliane nami kupitia njia ya arafa ukitumia nambari ifwatayo-: 0721 970 520. Au 020 2679842.Ikiwa unaishi Nairobi tunakukaribisha ututembelee kwenye studio zetu za TWR Kamburu Drive,off Ngong Road, baada ya jumba la TOP PLAZA.Anwani yangu ikiwa utaniandikia barua ni-:Kwa mtayarishi,Mwito,S.L.P.21514-00505 Nairobi.Waweza pia kuwasiliana nami kwa njia ya barua pepe ifwatavyo-barua@twr.co.ke.Na basi kufikia hapo sina budi kulikunja jamvi langu kwa leo ninapokutakia baraka sufufu kutoka kwake Mungu wetu mtukuka.Juma lijalo tutaingia aya ya 13 ya sura ya 8 ya kitabu cha Warumi.Ni mwaandazi wa kipindi hiki ndugu Charles Otunga ninayekuaga nikikutakia mbawazi zake Mungu wetu mtukuka.

Kwaheri.